TANGAZO LA SERIKALI Na. 221 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MATOGORO SHULE YA MWAKA 2023.

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Matogoro Shule ya Mwaka 2023.

Kutangaza Eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Kuandaa na kuhifadhi Mipangokina

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MH1 yenye majira - nukta 568737MS, 8811568KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $20^0$ 20'29'' kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi majumba saba kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MH2 yenye majira - nukta 568740MS, 8811896KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $88^0$ 06'05'' kwa umbali wa kilomita 1.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MH3 yenye majira - nukta 570388MS, 8812475KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $25^0$ 27'07'' kwa umbali wa kilomita 1.6 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MH4 yenye majira - nukta 571084MS, 8811004KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa $54^0$

33'15'' kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MH5 yenye majira - nukta 570638MS, 8810687KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa $78^0$ 41'24'' kwa umbali wa kilomita 1.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MH6 yenye majira - nukta 568787MS, 8810318KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa $01^0$ 28'50''kwa umbali wa kilomita 1.5 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*